

Maswali

1. Waisraeli walifanya nini iliyomkasirisha Mungu?
2. Nani walikuwa adui wa Waisraeli?
3. Wamidiani walifanyaje Waisraeli?
4. Waisraeli walifanya nini?
5. Mungu alichagua nani kuokoa Waisraeli?
6. Watu wangapi walikuwa kwa jeshi la Wamidiani? Wangapi walikuwa kwa jeshi la Waisraeli?
7. Gideoni aliwapa watu wake 300 nini?
8. Wale watu 300 walifanya nini katikati ya usiku?
9. Wamidiani walifanya nini?
10. Waisraeli walikuwa na amani nchini mwao kwa muda gani?

Majibu

1. Waisraeli walisahahu Mungu na wakaanza kuabudu sanamu.
2. Wamidiani walikuwa adui wao.
3. Wamidiani waliwaua, wakachoma mimea na nyumba zao.
4. Waisraeli waliomba Mungu awasamehe na awaokoe.
5. Mungu alichagua Gideoni kuwaokoa Waisraeli.
6. Maelfu ya watu kwa jeshi la Wamidiani, wengi sana hata hawahesabiki. Jeshi la Waisraeli lilikuwa na watu 300.
7. Gideoni aliwapea tarumbeta, mienge za moto na mitungi.
8. Waliende kwa kambi ya Wamidiani kwa vikundi 3 kwa eneo tofauti tofauti. Walipiga tarumbeta, wakavunja mitungi na mienge zao zikawashwa.
9. Wamidiani waliogopa na kuchanganyikiwa. Walipigana wenyewe kwa wenyewe na wakatoroka.
10. Waisraeli walikuwa na amani kwa miaka 40 kwa nchi yao.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



20 Gideoni

Marejeo

Waamuzi 6:1 – 14 na 7: 15 – 25

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu alijibu maombi ya Waisraeli. Waisraeli walijifunza .

Maneno maalum

- 20.1 Mungu + penda + Waisraeli + abudu sanamu + Wamidiani + jeshi kubwa + uawa + choma nyumba na mimea
- 20.2 Waisraeli + omba + Mungu anasamehe + Gideoni + waokoe
- 20.3 Jeshi la Wamidiani + maelfu + Gideoni + Jeshi la Waisraeli + watu 300 + Mungu atawaokoa
- 20.4 Usiku + watu 300 + vikundi 3 + tarumbeta + mwenge wa moto + mtungi
- 20.5 Gideoni + piga tarumbeta + vunja mitungi + mienge ya moto + Wamidiani + changanyikiwa + pigana wenyewe kwa wenyewe + toroka
- 20.6 Mungu aliokoa Waisraeli + shukuru Mungu + amani kwa miaka 40

20.1 Mungu aliwapenda Waisraeli na aliwasaidia wakati wote. Mungu aliwatoa kutoka Misri mpaka kwa nchi ya Kanaani kwa amani. Aliwasaidia kukaa kule. Lakini Waisraeli walikuwa waovu sana. Walisahahu Mungu. Waliabudu sanamu badala ya Mungu. Mungu aliudhika sana nao kwa sababu walimsahahu na hawakumpenda.

Waisraeli walikuwa na adui walioitwa Wamidiani. Wamidiani walikuwa na jeshi kubwa mno. Walikuja kwa nchi ya Waisraeli na wakaua watu na kuchoma makasi yao. Waisraeli waliogopa sana hata wakatoroka na kujificha kwenye mapango na msituni. Wamidiani waliwatafuta kwa nchi nzima. Waliua mifugo yao na kuchoma mimea zao. Waisraeli hawakupaki na cho chote cha kukula.

20.2 Waisraeli walikumbuka Mungu na vile aliwapenda na kuwalinda. Walisikitika kuwa walimsahahu na kuwa waovu. Kwa hivyo walianza kuomba Mungu. Waliuliza Mungu awasamehe na awaokoe kutoka kwa Wamidiani.

Kawaida Mungu ni wa upendo na ni mwema, aliwasamehe na akawasaidia. Kulikuwa na mtu aliyetitwa Gideoni, alipenda Mungu. Malaika alimkuja Gideoni na kumwambia kwamba atamsaidia kuokoa Waisraeli kutoka kwa Wamidiani.

20.3 Baada ya siku chache, Wamidiani walikusanyika pamoja ili wawapige Waisraeli. Gideoni alipiga tarumbeta ya kuwasanya Waisraeli pamoja ili awaongoze kupigana.

Gideoni aliongoza jeshi la Israeli mpaka kwa bonde fulani na wakapiga kambi kule. Jeshi la Wamidiani lilipiga kambi upande mwingine wa lile bonde. Jeshi la Gideoni lilikuwa na watu 32,000 lakini watu wa jeshi la Wamidiani halingeweza kusabuliwa kwa sababu walikuwa wengi sana.

Mungu alimwambia Gideoni kwamba alikuwa na watu wengi sana kwa jeshi lake. Ikiwa Mungu alikuwa anawapigania, walitakiwa watu wachache tu. Watu 22,000 waliogopa na kurudi nyumbani. Mungu aliambia Gideoni aendelee kupunguza watu. Kwa hivyo alipunguza na akabaki na watu 300 pekee wa kupigana na maelfu ya Wamidiani.

20.4 Usiku huo ilipokuwa giza sana, Gideoni alikusanya watu wake 300 pamoja. Aliomba Mungu ili awasaidie. Gideoni aligawanya watu wake kwa vikundi 3 vya watu 100 kwa kila kikundi. Alipea kila mtu tarumbeta, mwenge wa moto na mtungi. Aliwambia watakachofanya.

Wale watu 300 walitambaa polepole mpaka wakavuka lile bonde. Walizificha tarumbeta zao na mienge ndani ya mitungi. Walipofika kwa kambi ya Wamidiani, vile vikundi 3 kila kimoja kilienda eneo lake – waligawanyika. Kila kikundi kilienda upande wake wa kambi ya Wamidiani. Walichificha msituni na kuongoja ishara ya Gideoni. Jeshi la Wamidiani walikuwa wamelala fofoofo.

20.5 Bunde tu Gideoni aliruka juu na watu wote. Walipiga tarumbeta kwa sauti kuu. Walivunja mitungi kwa kishindo na kumlika mienge yao kutoka kwa kila upande wa kambi ya Wamidiani. Walipiga tarumbeta tena kwa sauti kubwa na kutoa sauti zaidi iwezekanavyo, wakisema, “Upanga wa Bwana na wa Gideoni.”

Wamidiani waliamka. Walitoka kwa mahema na hawakuelewa kilichotokea. Walichanganyikiwa kwa kelele na mwangaza uliozunguka kambi yao.

Gideoni na watu wake waliangalia na kusikiliza kelele iliyojaa. Mungu alifanya Wamidiani wafikirie kwamba Waisraeli walikuwa na jeshi kubwa iliyokuwa ikipigana nao kwa sababu ya tarumbeta, mwangaza na kelele kuu.

Kwa sababu ya giza na kuchanganyikiwa, Wamidiani walianza kupigana na kuuana wenyewe kwa wenyewe. Wote waliogopa na kuanza kutoroka. Gideoni na watu wake waliwafuguza na kuua wana wa kifalme wawili.

20.6 Kwa hivyo Mungu alisaidia Gideoni akashinda Wamidiani na kuokoa Waisraeli. Waisraeli walishukuru Mungu sana kwa kuwaokoa. Waliacha kuabudu sanamu na wakapenda Mungu na kumtii. Mungu alifurahi sana kwa sababu Waisraeli walimpenda tena. Aliwapa amani kutoka kwa adui wao kwa miaka arobaini.